JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# MWONGOZO WA KITAIFA WA BIASHARA YA KABONI

OKTOBA, 2022


## DIBAJI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoathiriwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa isiyotabirika. Hali hii inajidhihirisha kupitia matukio mvua zisizotabirika, ongezeko la joto, ukame na mafuriko. Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeathiri sekta za kijamii na kiuchumi na maendeleo kama vile kilimo, utalii, nishati, maji, afya, mifugo na mifumo ikolojia ya bahari na hivyo kuathiri ongezeko la pato la taifa. Ukame na mafuriko yamechangia gharama kubwa za kiuchumi, kuathiri maendeleo na maisha ya jamii za vijijini na mijini kwa pande zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali inatakiwa kuweka utaratibu wa kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi ili kulinda maendeleo yaliyofikiwa na kufikia maendeleo endelevu. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, jitihada hizo ni pamoja na; mapitio ya sera, uandaaji wa kanuni, mikakati na miongozo ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi hufanyika katika sekta za nishati, usafirishaji, udhibiti wa taka, misitu, kilimo, shughuli za uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa pamoja na matumizi mengine ya ardhi. Inatarajiwa kuwa, miradi ya biashara ya kaboni inayotekelezwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika sekta hizo itachangia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kuchangia katika utunzaji endelevu ya mazingira na kuleta maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Hivyo, Mwongozo huu unakusudia kuweka taratibu na matakwa kitaifa katika kusimamia na kudhibiti miradi ya biashara ya kaboni nchini.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kusimamia kwa ufanisi malengo ya Mwongozo huu na kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wa kimataifa, kikanda na kitaifa wanaojihusisha na miradi ya biashara ya kaboni. Hivyo, natoa wito kwa wadau wote kuzingatia Mwongozo huu katika kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni.



Dkt. Selemani Said Jafo (Mb)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS**
**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**

## SHUKURANI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Biashara ya Kaboni kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia biashara ya kaboni. Mwongozo huu unakusudia kutumia fursa zinazohusiana na biashara ya kaboni kulingana na taratibu zilizoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto, Makubaliano ya Paris na masoko huria ya miradi ya biashara ya kaboni.

Maandalizi ya Mwongozo huu yasingefanikiwa bila ushirikiano na dhamira ya dhati kutoka kwa wadau wakiwemo wataalamu kutoka sekta za umma na binafsi, taasisi za kitaaluma pamoja na asasi za kiraia. Nitumie fursa hii kutambua michango na jitihada zao muhimu zilizofanikisha maandalizi ya Mwongozo huu.

Kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ya Norway kupitia Ubalozi wa Kifalme wa Norway, Dar es Salaam kwa msaada wa rasilimali fedha katika maandalizi ya Mwongozo huu kupitia Mpango wa Utayari wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.
Ni matumaini yangu kwamba Mwongozo huu unaweka mazingira wezeshi kwa wadau wanaojihusisha na miradi ya biashara ya kaboni katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mary N. Maganga
**KATIBU MKUU**
**(OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA)**

## TABLE OF CONTENTS

DIBAJI ..... i
TABLE OF CONTENTS ..... iii
FAHARASA ..... iv
SURA YA KWANZA ..... 1
1.0 UTANGULIZI ..... 1
1.1 Usuli ..... 1
1.2 Madhumuni na Misingi ya Biashara ya Kaboni ..... 1
1.2.1 Madhumuni ..... 1
1.2.2 Misingi ..... 1
1.3 Malengo ..... 2
1.4 Mawanda ya Mwongozo ..... 2
1.5 Umuhimu wa Mwongozo wa Biashara ya Kaboni ..... 2
SURA YA PILI ..... 3
2.0 SEKTA MUHIMU KATIKA BIASHARA YA KABONI ..... 3
2.1 Sekta ya Nishati ..... 3
2.2 Sekta ya Usafirishaji ..... 3
2.3 Udhibiti wa Taka ..... 3
2.4 Sekta ya Misitu ..... 4
2.5 Sekta ya shughuli za uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa ..... 4
2.6 Sekta ya Kilimo ..... 5
2.7 Matumizi mengine ya Ardhi ..... 5
SURA YA TATU ..... 6
3.0 MATAKWA NA TARATIBU ZA BIASHARA YA KABONI ..... 6
3.1 Matakwa ya miradi ya biashara ya kaboni ..... 6
3.1.1 Matakwa ya Mpendekezaji ..... 6
3.1.2 Matakwa ya mradi ..... 6
3.1.3 Tathmini ya Athari kwa Mazingira ..... 6
3.2 Hatua za kufuata katika kuanzisha na kendesha mradi wa biashara ya kaboni ..... 7
3.2.1 Taratibu za maombi ..... 7
3.3 Vipengele vya Andiko la Awali la Mradi na Andiko la Mradi ..... 8
3.3.1 Andiko la Awali la Mradi ..... 8
3.3.2 Andiko la Mradi ..... 8
3.4 Vipengele vya mkataba ..... 8
3.5 Kufutwa kwa Idhini ya Mradi ..... 9
SURA YA NNE ..... 10
4.0 MGAWANYO WA GHARAMA NA FAIDA KATIKA BIASHARA YA KABONI ..... 10
4.1 Mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida za biashara ya kaboni ..... 10
4.1.1 Mmiliki ..... 10
4.1.2 Mpendekezaji wa Mradi ..... 10
4.1.3 Mamlaka za Udhibiti ..... 10
4.1.4 Jamii zinazozunguka eneo la mradi ..... 11
4.2 Mgawanyo wa gharama na faida miongoni mwa wadau katika biashara ya kaboni ..... 11
4.2.1 Mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida Tanzania Bara ..... 11
4.2.2 Mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida Zanzibar ..... 12
SURA YA TANO ..... 13
5.0 MFUMO WA KITAASISI ..... 13
VIAMBATISHO ..... 14

## FAHARASA

**Andiko la Mradi** maana yake ni andiko lenye maelezo ya kina kuhusu mradi wa biashara ya Kaboni;

**Baraza** maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria;

**Biashara ya Kaboni** maana yake ni kuuza na kununua Viwango vya Kaboni viliyoidhinishwa au kuthibishwa katika utoaji, upunguzaji na uondoaji wa kaboni kwa mujibu wa Viwango vya Kaboni vinavyotambulika kimataifa;

**Gesijoto** maana yake ni gesi zilizo katika angahewa zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi;

**Kanuni** maana yake ni Kanuni za Usimamizi wa Mazingira kuhusu udhibiti na usimamizi wa Biashara ya Kaboni;

**Kuepuka upotevu na uharibifu wa misitu** maana yake ni kuepuka upotevu wa misitu unaosababishwa na kubadilishwa kwa matumizi ya ardhi kwenda kwenye matumizi mengine yanayoondoa uoto wa misitu, au kuepuka shughuli zinazoharibu misitu bila kusababisha upotevu wa misitu wa moja kwa moja;

**Mabadiliko ya tabianchi** maana yake ni mabadiliko ya muda mrefu ya mifumo ya hali ya hewa inayohusishwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na shughuli za binadamu;

**Mamlaka ya Uratibu** maana yake ni Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa au Mamlaka ya Kitaifa.

**Mamlaka ya Usimamizi** maana yake ni taasisi yoyote ya serikali yenye jukumu la kusimamia mazingira na mabadiliko ya tabianchi Zanzibar;

**Mamlaka za Udhibiti** maana yake ni taasisi za serikali zinazohusika na kuhamasisha uwekezaji, usajili wa biashara na leseni, benki, ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa mazingira, viwango, soko la hisa, tawala za mikoa, wizara za sekta husika, idara na wakala;

**Mfumo wa Mgawanyo wa Gharama na Faida** maana yake ni mfumo unaotumika kugawa gharama na faida kwa wadau katika miradi ya Biashara ya Kaboni;

**Mkurugenzi** maana yake ni mkurugenzi wa mazingira aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria;

**Mmiliki** maana yake mmiliki wa mali inayohusika katika Biashara ya Kaboni;

**Mpendekezaji** maana yake ni mtu yeyote awe wa kisheria au halisi anayependekeza au anayehusika na utekelezaji wa mradi au programu ya Biashara ya Kaboni;

**Mradi wa Kaboni** maana yake ni mradi wowote unaotekelezwa kwa ajili ya kuzalisha Viwango vya Kaboni vinavyotambulika kimataifa;

**Msajili** maana yake ni Mamlaka ya Uratibu yenye jukumu la kusajili miradi ya biashara ya kaboni Tanzania Bara na Zanzibar;

**REDD+** maana yake ni kupunguza utoaji wa gesijoto kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu na kutekeleza jukumu la uhifadhi, usimamizi endelevu na kuongeza kiasi cha kaboni ya misitu katika nchi zinazoendelea;

**Sheria** maana yake ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191;

**Soko Huria la Kaboni** maana yake ni mfumo wa biashara ya kaboni usiosimamiwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi;

**Upandaji Miti** maana yake ni kupanda miti kwenye ardhi ambayo kihistoria haijawahi kuwa na misitu;

**Upandaji Miti Upya** maana yake ni kupanda miti ili kurudisha msitu kwenye ardhi ambayo kihistoria kulikuwa na msitu;

**Uzalishaji wa Gesijoto** maana yake ni uzalishaji wa gesijoto katika angahewa kwa kipindi cha muda maalumu;

**Viwango vya Kaboni** maana yake kiasi cha tani moja ya hewa ya kabonidayoksaidi au kiasi kinacholinga na hicho cha hewa nyingine ya gesijoto kinachopunguzwa kwa ajili ya kuuzwa kwenye Biashara ya Kaboni.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Usuli

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 1992; Itifaki ya Kyoto ya mwaka 1997; na Makubaliano ya Paris ya mwaka 2015. Mikataba hii pamoja na mambo mengine inatoa utaratibu kwa nchi wanachama kutimiza wajibu wao wa kupunguza uzalishaji wa gesijoto lakini pia kufaidika na miradi ya biashara ya kaboni.

Mwongozo wa kwanza wa Kitaifa wa Biashara ya Kaboni uliandaliwa mwaka 2016 ili kutoa mwongozo kuhusu ya miradi ya biashara ya kaboni kwa sekta zote kulingana na utaratibu wa miradi ya maendeleo na upunguzaji wa gesijoto chini ya Itifaki ya Kyoto. Hata hivyo, Makubaliano ya Paris ya 2015 yalianzisha utaratibu mpya wa biashara ya kaboni ambao unahimiza nchi wanachama kuchukua hatua za kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizi ni pamoja na kupunguza utoaji wa gesijoto kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu na kutekeleza jukumu la uhifadhi, usimamizi endelevu na kuongeza kiasi cha kaboni ya misitu katika nchi zinazoendelea (REDD+), ushirikiano wa hiari, mbinu za ushirikiano na mbinu zisizo za soko baina ya nchi wanachama.

Aidha, Makubaliano ya Paris yanazitaka nchi wanachama kuandaa, kuwasilisha na kutekeleza Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ambao unapaswa kufuatwa kwa kutumia hatua za ndani za nchi husika za kukabiliana na kuhimili na mabadiliko ya tabianchi ili kuhamasisha maendeleo endelevu. Kwa muktadha huu, kwa mara ya kwanza Tanzania iliandaa na kuwasilisha Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi mwaka 2021.

Ili kuendana na mifumo iliyopo na mipya ya kimataifa ya Viwango vya Kaboni, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepitia na kuandaa Sera zake za Kitaifa za Mazingira, mikakati na mipango ya mabadiliko ya tabianchi ikijumuisha Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032). Nyaraka hizi za kisera zinawezesha utekelezaji wa biashara ya kaboni na mifumo mingine ya soko inayoibuka chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris. Hivyo, Mwongozo wa Taifa wa Biashara ya Kaboni (2022) umeandaliwa ili kujumuisha masuala yote muhimu kuhusu Biashara ya Kaboni na mifumo mingine ya Biashara ya Kaboni inayoibuka.

### 1.2 Madhumuni na Misingi ya Biashara ya Kaboni

#### 1.2.1 Madhumuni

Madhumuni ya Mwongozo huu ni kuimarisha mchango wa nchi katika jitihada za kupunguza uzalishaji wa gesijoto na hivyo kupunguza athari za mazingira kwa kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

#### 1.2.2 Misingi

Mwongozo huu umejikita kwenye misingi muhimu ifuatayo: maendeleo endelevu, utunzaji endelevu wa mazingira, ushiriki wa jamii, uwazi, ufanisi, ujumuishaji wa faida za kijamii, kiuchumi na mazingira, na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa.

## 1.3 Malengo

Lengo la jumla la Mwongozo huu ni kutoa taratibu na matakwa ya kitaifa ya kufanya miradi ya biashara ya kaboni Tanzania Bara na Zanzibar.

Malengo mahususi

a) Kutoa na kubainisha taratibu na matakwa ya uwazi katika kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni;
b) Kutoa mwongozo wa mgawanyo wa gharama na faida katika faida katika miradi ya biashara ya kaboni;
c) Kuainisha mifumo ya kitaasisi na kiutawala katika kuendesha miradi ya biashara ya kaboni; na
d) Kujenga uelewa kwa wawekezaji, watoa uamuzi na wadau wengine kuhusu fursa za biashara ya kaboni katika sekta mbalimbali.

## 1.4 Mawanda ya Mwongozo

Mwongozo huu unaweka taratibu na masharti ambayo wadau na wajasiriamali wa biashara ya kaboni watapaswa kuzingatia wakati wa utekelezaji wa miradi mipya na inayoendelea ya biashara ya kaboni katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwongozo huu unaendana na sera husika na mifumo ya kisheria ambayo inapaswa kuzingatiwa na inaanisha sekta muhimu katika Biashara ya Kaboni nchini.

## 1.5 Umuhimu wa Mwongozo wa Biashara ya Kaboni

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea zenye fursa nyingi kwenye sekta zinazoweza kushiriki katika miradi ya Biashara ya Kaboni kwa lengo la kuchangia juhudi za kimataifa katika kupunguza uzalishaji wa gesijoto sambamba na kuimarisha uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi nchini. Kabla ya kuandaliwa kwa Mwongozo na Kanuni, miradi ya biashara ya kaboni ilikuwa ikiendeshwa nchini bila kudhibitiwa. Usimamizi bora na wenye ufanisi wa biashara ya kaboni unahitaji mfumo wa kisera na kisheria kuongoza na kuwezesha watendaji na wadau wengine husika kushiriki kwa usawa katika biashara hii. Kwa kutambua ukweli huu na fursa iliyopo, Serikali imeandaa Kanuni na Mwongozo kwa ajili ya kuweka mfumo wa kisheria, kitaasisi na kiutawala wa kudhibiti na kusimamia uendeshaji wa miradi ya biashara ya kaboni nchini. Nyaraka hizi za kisera zinawezesha utekelezaji wa biashara ya kaboni na mifumo mingine ya soko inayoibuka chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na masoko huria ya kaboni kwa sekta zote muhimu.

Aidha, Mwongozo huu unaendana na Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni) za 2022, Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032), Sera ya Mazingira ya Zanzibar (2013), Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi Zanzibar (2014-2030) na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ya mwaka 2015.

Mwongozo huu unalenga kuwawezesha wadau kufanya biashara ya kaboni kwa usahihi kwa njia inayofahamika zaidi, ya uwazi na iliyoratibiwa. Pia unatarajiwa kujenga uelewa kuhusu fursa zilizopo za biashara ya kaboni.

# SURA YA PILI

## 2.0 SEKTA MUHIMU KATIKA BIASHARA YA KABONI

Mifumo ya kisera na kisheria hususan Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, unaainisha sekta za kipaumbele na hatua za kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi nchini. Sekta za kipaumbele zilizoainishwa ili kufikia malengo ya kitaifa ya kupunguza uzalishaji wa gesijoto ni nishati, uchukuzi, misitu na udhibiti wa taka. Sekta nyingine muhimu ni pamoja na uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa, kilimo na matumizi mengine ya ardhi.

### 2.1 Sekta ya Nishati

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina vyanzo vingi vya nishati. Hata hivyo, vyanzo hivi havijatumika ipasavyo hivyo kwa kiasi kikubwa sekta hii inategemea vyanzo vya nishati visivyo rafiki wa mazingira. Matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati hutoa fursa kubwa kwa biashara ya kaboni.

Maeneo yenye fursa za uwekezaji wa biashara ya kaboni katika sekta hii ni pamoja na:

a) Matumizi ya vyanzo vya nishati safi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme kama vile joto ardhi, upepo, mawimbi, jua, matumizi ya gesi asilia, umeme unaotokana na maji na tungamotaka;
b) Kuongeza matumizi ya gesi asilia kwa ajili kupikia na matumizi mengine ya nyumbani kupitia uboreshaji wa mifumo ya usambazaji wa gesi asilia kote nchini;
c) Kuhamasisha upatikanaji wa teknolojia nafuu na zenye ufanisi za nishati;
d) Kuhamasisha shughuli za uzalishaji wa nishati jumuishi kama vile kuzalisha kwa pamoja joto na nishati; na
e) Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya nishati.

### 2.2 Sekta ya Usafirishaji

Ukuaji wa uchumi nchini katika kipindi cha miongo iliyopita umechochea ongezeko la matumizi ya vyombo vya usafiri vinavyotumia nishati ya mafuta. Matokeo yake sekta hii inachangia uzalishaji wa gesijoto wa jumla kitaifa na hivyo kutoa fursa ya kupunguza gesijoto kupitia miradi ya biashara ya kaboni.

Maeneo yenye fursa za uwekezaji wa biashara ya kaboni katika sekta hii ni pamoja na:

a) Matumizi ya nishati safi katika vyombo vya usafirishaji;
b) Mifumo ya Usafiri wa Umma wa Haraka;
c) Usafiri usio wa vyombo vya moto; na
d) Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya usafirishaji.

### 2.3 Udhibiti wa Taka

Udhibiti wa taka ngumu na maji taka unahusisha wadau mbalimbali kuanzia uwekezaji wa kiteknolojia na usimamizi wa kitaalamu wa mitambo. Ukusanyaji,

uhifadhi, usafirishaji, kutibu, kutupa, pamoja na kurejeleza hutoa fursa kwa biashara ya kaboni nchini.

Viwango vya juu vya gesi ya methani miongoni mwa gesijoto nyingine zinazozalishwa hutokana na kuoza kwa taka na hivyo kuongeza viwango vya uzalishaji wa gesijoto. Kwa upande mwingine, gesi ya methani pia inaweza kutumika kama chanzo cha nishati na hivyo kutoa fursa ya miradi ya biashara ya kaboni.

Maeneo yenye fursa za uwekezaji wa biashara ya kaboni katika sekta hii ni pamoja na:
a) Matumizi ya njia za kisasa za kudhibiti taka ikiwa ni pamoja na kuimarishwa kwa matumizi ya uvunaji wa methani kutoka kwenye madampo;
b) Uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia za kuzalisha nishati kutokana na taka;
c) Uvunaji wa methani unaotokana na kutibu maji taka; na
d) Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya usimamizi wa taka.

## 2.4 Sekta ya Misitu

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina rasilimali nyingi za misitu. Hata hivyo, sehemu kubwa ya nchi inakabiliwa au kutishiwa na uharibifu wa mazingira ya misitu na mifumo ya ikolojia ya bahari. Kwa mantiki hiyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina nafasi kubwa ya kushiriki katika miradi ya biashara ya kaboni inayotegemea misitu. Miradi ya biashara ya kaboni chini ya sekta ya misitu inaweza kutekelezwa kupitia misitu chini ya serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa, vijiji, jamii na sekta binafsi.

Maeneo yenye fursa za uwekezaji wa biashara ya kaboni katika sekta hii ni pamoja na:
a) Kupunguza uzaishaji wa gesijoto kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu;
b) Kuimarisha usimamizi wa misitu;
c) Uhifadhi wa misitu;
d) Upandaji Miti au Upandaji Miti Upya;
e) Urejeshaji wa mifumo ya ikolojia iliyoharibika;
f) Fursa za kaboni ya bluu kama vile uhifadhi wa mikoko, nyasi za baharini, maji ya chumvi, pamoja na shughuli nyingine za uchumi wa bluu zinazofyonza kaboni kutoka angani; na
g) Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya misitu.

## 2.5 Sekta ya shughuli za uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanzisha shughuli za ujenzi wa viwanda kuelekea uchumi wa kati ambao pamoja na mambo mengine unategemea kwa kiasi kikubwa matumizi ya malighafi na rasilimali za nishati. Hivyo, kuna fursa ya kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni katika sekta hii kwa lengo la kuwa na kiwango cha chini cha gesijoto kupitia mbinu na teknolojia bora ya uzalishaji.
Maeneo yenye fursa za uwekezaji wa biashara ya kaboni katika sekta hii ni pamoja na:
a) Matumizi ya mbinu na teknolojia bora za uzalishaji;
b) Vyanzo anuai vya nishati na matumizi ya nishati mbadala;
c) Udhibiti wa taka za viwandani; na

d) Uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya shughuli za uzalishaji viwandani na matumizi ya bidhaa.

### 2.6 Sekta ya Kilimo

Sekta ya kilimo ni kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, na usalama wa chakula katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, sekta hii imeathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa.

Maeneo yenye fursa za uwekezaji wa miradi ya biashara ya kaboni katika sekta hii ni pamoja na matumizi ya mbinu za Kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kama vile kuboreshwa kwa kilimo cha ukwatuaji, udhibiti wa mmomonyoko wa udongo, matandazo, matumizi ya mbolea, uzalishaji bora wa chakula, usimamizi wa malisho, uvunaji wa maji, kilimo cha uhifadhi, kilimo mseto, kufunika mazao, ufugaji wa samaki jumuishi na ujumuishaji wa nishati ya biogesi katika mashamba na uwekezaji mwingine unaolenga kupunguza uzalishaji wa gesijoto katika sekta ya kilimo.

### 2.7 Matumizi mengine ya Ardhi

Matumizi mengine ya ardhi ambayo yanaweza kuwa na sifa za uwekezaji wa miradi ya biashara ya kaboni ni pamoja na usimamizi bora wa nyasi, udhibiti bora wa moto pori, uboreshaji wa maeneo ya malisho na ardhi nyingine zilizoharibika.

## SURA YA TATU

## 3.0 MATAKWA NA TARATIBU ZA BIASHARA YA KABONI

Sura hii inaelezea matakwa na taratibu za kufuata katika kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni Tanzania Bara na Zanzibar. Matakwa na taratibu hizi zinazingatia kanuni za udhibiti na usimamizi wa biashara ya kaboni.

### 3.1 Matakwa ya miradi ya biashara ya kaboni

#### 3.1.1 Matakwa ya Mpendekezaji

Mpendekezaji na Wabia washirika katika kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni watapaswa kutambulika kisheria kwa mujibu wa sheria za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mpendekezaji anatakiwa kuzingatia matakwa yafuatayo:

a) Kuwa na utaalamu mahususi wa biashara ya kaboni;
b) Awe amesajiliwa na Mamlaka za Usimamizi;
c) Kuwa na uwezo wa kifedha wa kuwekeza katika miradi ya biashara ya kaboni; na
d) Matakwa mengine ya kisheria katika kufanya biashara ya miradi ya kaboni nchini.

#### 3.1.2 Matakwa ya mradi

Mtu yeyote anayekusudia kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapaswa kusajiliwa na Msajili kabla ya kuanza kutekeleza mradi.

Mradi unaotakiwa kusajiliwa kama mradi wa biashara ya kaboni, utakuwa na sifa zifuatazo: -

a) Uwe unaendana na sera, sheria na mikakati ya kitaifa;
b) Uonyeshe jinsi mradi utakavyo changia katika Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi;
c) Kuzingatia sekta za kipaumbele za kitaifa katika biashara ya kaboni;
d) Barua ya ridhaa na kushiriki kwa wabia wanaohusika katika mradi;
e) Uthibitisho wa umiliki wa mali inayohusika katika mradi;
f) Kushirikisha jamii zinazozunguka mradi katika utekelezaji wa mradi;
g) Kuzingatia uwazi na haki katika biashara;
h) Kuzingatia vipaumbele vya kitaifa katika uwekezaji, ulinzi wa ikolojia, jamii utamaduni na uchumi;
i) Kuweka wazi taarifa za msingi za mradi ikiwa ni pamoja na gharama, viwango vya kaboni vilivyothibitishwa na makisio ya mapato;
j) Kuonyesha fursa za ajira zinazotarajiwa kwa wataalamu wa ndani ya nchi na jamii zinazozunguka mradi; na
k) Kuonyesha mradi utakavyowajibika katika utoaji wa huduma kwa jamii.

#### 3.1.3 Tathmini ya Athari kwa Mazingira

Miradi ya biashara ya kaboni itatakiwa kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira na jamii kwa mujibu wa Kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na sheria nyingine zinazohusika. Pamoja na hayo, miradi inayohusiana na kupunguza uzalishaji wa gesijoto kutokana na upotevu na uharibifu wa misitu, na jukumu la uhifadhi,

usimamizi endelevu na kuongeza kiasi cha kaboni ya misitu katika nchi zinazoendelea, inatakiwa kufanyiwa tathmini ya viwango vya REDD+.

### 3.2 Hatua za kufuata katika kuanzisha na kendesha mradi wa biashara ya kaboni

#### 3.2.1 Taratibu za maombi

Mtu anayekusudia kutekeleza miradi ya biashara ya kaboni anapaswa kufuata hatua zifuatazo:

1. Kuwasilisha maombi ya kuidhinishwa kwa wazo la mradi kwa Mamlaka ya Usimamizi kwa kujaza fomu ya maombi inayoambatana na malipo ya ada ya maombi isiyorejeshwa kama ilivyoainishwa katika kanuni.

Nini cha kufanya?

a) Kamilisha fomu ya maombi kama ilvyoainishwa katika kanuni;
b) Wasilisha fomu ya maombi iliyokamilika ikiambatana na uthibitisho wa malipo ya ada za maombi kwa mujibu wa kanuni; na
c) Subiri majibu ya usajili wa wazo la mradi ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa maombi.

2. (a) Kuandaa na kuwasilisha Andiko la Awali la Mradi likiambatana na idhini ya Mmiliki kwa njia ya dondoo za muhtasari ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya usajili wa wazo la mradi.

   (b) Lipa ada ya usajili kwa mujibu wa kanuni.

Nini cha kufanya?

a) Shirikiana na Mmiliki kuandaa Andiko la Awali la Mradi;
b) Pata idhini ya Mmiliki ya kutekeleza mradi katika eneo lake;
c) Wasilisha Andiko la Awali la Mradi likiambatana na uthibitisho wa malipo ya ada ya usajili wa mradi kwa mujibu wa kanuni; na
d) Subiri majibu ya Andiko la Awali la Mradi ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa andiko.

3. Kuandaa Andiko la Mradi kwa mujibu wa viwango stahiki vya kimataifa ndani ya miezi 12 baada ya kupata barua ya kutokuwa na pingamizi.

Nini cha kufanya?

a) Shirikiana na Mmiliki kuandaa Andiko la Mradi; na
b) Wasilisha Andiko la Mradi kwa mujibu wa viwango stahiki vya kimataifa.

4. Wasilisha Andiko la Mradi lillliloandaliwa kwa mamlaka ya Usimamizi kwa ajili ya kupata idhini.

Nini cha kifanyike?

a) Mamlaka ya Usimamizi itapitia na kuchambua Andiko la Mradi ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya kupokelewa; na
b) Kutoa Barua ya Kuidhinishwa kwa mradi uliopitishwa.

5. Kuanza kutekeleza shughuli za mradi ndani ya miaka miwili baada ya kupokea Barua ya idhini.

Nini cha kufanya?
a) Toa taarifa kwa Mamlaka ya Usimamizi kuhusu kuanza kwa mradi;
b) Wasilisha ripoti ya maendeleo ya mradi ya kila mwaka kwa Mamlaka ya Usimamizi;
c) Wasilisha nakala za ripoti ya mkaguzi wa nje ya kila mwaka kwa miaka mitano

### 3.3 Vipengele vya Andiko la Awali la Mradi na Andiko la Mradi

Pale ambapo Mpendekezaji wa mradi anatakiwa kuandaa Andiko la Awali la Mradi na Andiko la Mradi, nyaraka hizo zitakuwa na vipengele kama inavyoonyeshwa hapa chini.

#### 3.3.1 Andiko la Awali la Mradi

Andiko la Awali la Mradi lililoandaliwa na Mpendekezaji litakuwa na vipengele vifuatavyo:
a) Jina la mradi;
b) Jina na mawasiliano ya Mpendekezaji;
c) Maelezo mafupi ya mradi;
d) Shughuli zinazopendekezwa;
e) Wadau watakaohusika;
f) Eneo la mradi linalopendekezwa, mahali na ukubwa;
g) Faida zinazotarajiwa za mradi;
h) Vyanzo vya fedha na makadirio ya gharama za uwekezaji;
i) Utaratibu wa malipo au mfumo wa ulipaji wa viwango vya kaboni; na
j) Uzingatiaji wa mazingira na kudhibiti faida za kijamii na kiuchumi.

#### 3.3.2 Andiko la Mradi

Pamoja na vipengele vilivyopo kwenye Andiko la Awali, Andiko la Mradi litajumuisha vipengele vifuatavyo:
a) Maelezo ya jumla ya shughuli za mradi;
b) Maelezo ya kina ya takwimu za msingi na mbinu za ufuatiliaji;
c) Muda wa utekelezaji wa shughuli za mradi; na
d) Kipindi cha uzalishaji wa viwango vya kaboni.

### 3.4 Vipengele vya mkataba

Watu wanaokusudia kushirikiana katika miradi ya biashara ya kaboni wataingia mikataba ya makubaliano. Mkataba wowote utakaoingiwa utajumuisha:
a) Majina ya wahusika;
b) Anwani na mawasiliano ya wahusika;
c) Uwezo wa kisheria wa wahusika;
d) Maelezo na mawanda ya mradi;
e) Mawanda ya mkataba;
f) Vigezo na masharti ya wahusika;
g) Utaratibu wa mgawanyo wa gharama na faida za mradi;
h) Mfumo wa malipo ya mapato na faida iliyopatikana;
i) Uendeshaji na muda wa mradi;
j) Ukiukwaji wa masharti;

k) Utatuzi wa migogoro;
l) Sheria itakayotumika;
m) Marekebisho;
n) Kusimamisha na kuvunja;
o) Dhana ya majanga yasiyosababishwa na upande wowote;
p) Saini na mamlaka ya watiasaini;
q) Saini za mashahidi wa watiasaini; na
r) Lakiri au muhuri wa wahusika.

### 3.5 Kufutwa kwa Idhini ya Mradi

Mazingira yanayoweza kusababisha kufutwa kwa idhini ya mradi yatajumuisha:
a) Kushindwa kuwasilisha Andiko la Awali la Mradi au Andiko la Mradi ndani ya muda ulioainishwa;
b) kushindwa kuanza kwa shughuli za mradi ndani ya muda ulioainishwa;
c) Kutozingatia matakwa ya mradi kama yalivyoainishwa katika Kanuni hizi;
d) Mpendekezaji kufuta mradi kwa hiari yake kwa kutoa taarifa rasmi;
e) Pale ambapo idhini ilipatikana kwa udanganyifu;
f) Pale ambapo kuendelea kwa shughuli za mradi kuna au kunaweza kuwa na madhara kwa mazingira au afya ya binadamu;
g) Pale ambapo shughuli za mradi zinaathiriwa na maslahi mengine ya umma; na
h) Kutokuwepo au kuficha taarifa wakati wa mchakato wa maombi.

## SURA YA NNE

## 4.0 MGAWANYO WA GHARAMA NA FAIDA KATIKA BIASHARA YA KABONI

### 4.1 Mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida za biashara ya kaboni

Miradi ya biashara ya kaboni inakusudiwa sio tu kuhamasisha utunzaji endelevu wa mazingira bali pia kuongeza uhaulishaji wa teknolojia na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Viwango vya Kaboni vitatumika kufidia gesijoto au kuziwezesha taasisi au nchi kutimiza wajibu wao wa kupunguza uzalishaji wa gesijoto chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Itifaki ya Kyoto, Makubaliano ya Paris au mifumo ya soko huria.

Faida za kiuchumi zinahusisha uzalishaji wa mapato yanayotokana na uuzaji wa Viwango vya Kaboni kwa wadau wanaokusudia kupunguza viwango vya gesijoto. Miradi ya biashara ya kaboni huzalisha fedha ambazo zinaweza kutumika kuboresha mazingira safi kwa umma, afya na maendeleo endelevu na huduma za kijamii. Wadau wanaoweza kunufaika na biashara ya kaboni wamebainishwa hapa chini.

#### 4.1.1 Mmiliki

Kwa ujumla, miradi ya biashara ya kaboni inaweza kuhusisha matumizi ya ardhi au miradi mingine. Mmiliki anayetekeleza miradi ya biashara ya kaboni inayohusisha matumizi ya ardhi atalazimika kuachana na matumizi ambayo amekuwa akiyafanya na kimsingi yalikuwa muhimu kwa rasilimali hiyo. Katika aina hii ya miradi, Mmiliki anayemiliki ardhi na rasilimali nyingine zinazohusiana na ardhi hiyo itakuwa ndiyo mchango wake kwenye mradi na hivyo kuwa msingi wa mgawanyo wa mapato. Aidha, ambapo Mmiliki anashirikiana na Mpendekezaji wa Mradi, Mmiliki atachangia hisa ambazo zinajumuisha thamani ya ardhi wakati Mpendekezaji atawekeza katika kuendeleza mradi. Katika mazingira haya, Mmiliki atakuwa na hisa nyingi za Viwango vya Kaboni vilivyouzwa. Mbali na matumizi mengine ya maendeleo, kiasi cha fedha kutoka kwenye hisa za Mmiliki kitatumika kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali hiyo.

Kuhusu Miradi ya aina nyingine kama vile udhibiti wa taka, nishati na usafirishaji, gharama za awali za uwekezaji zinaweza kuwa juu. Katika mazingira haya, mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida utaamuliwa kwa makubaliano kati ya Mmiliki na Mpendekezaji wa mradi kwa kushauriana na Mamlaka ya Usimamizi.

#### 4.1.2 Mpendekezaji wa Mradi

Mpendekezaji wa Mradi ataingia gharama za kuandaa mradi na pia anaweza kuwezesha utekelezaji wa mradi. Vilevile, Mpendekezaji wa Mradi anatarajiwa kunufaika na uuzaji wa Viwango vya Kaboni kwa mujibu wa kanuni.

#### 4.1.3 Mamlaka za Udhibiti

Taasisi muhimu zinazohusika na kusimamia miradi ya biashara ya kaboni ni pamoja na taasisi zilizopewa mamlaka ya usimamizi wa mazingira, tawala za mikoa na serikali za mitaa na wizara za kisekta. Wakati wa kufanya uamuzi wa mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida, taasisi hizi zitazingatia kuwa zitakusanya ada na tozo zinazohusiana na kusimamia miradi ya biashara ya kaboni kwa mujibu wa sheria za nchi.

#### 4.1.4 Jamii zinazozunguka eneo la mradi

Miradi ya biashara ya kaboni ambayo haisimamiwi na jamii inatakiwa kuonyesha wazi jinsi jamii zinazozunguka eneo la mradi zinavyoweza kushiriki na kunufaika kutokana na mradi husika. Licha ya ushiriki wa moja kwa moja wa jamii, mradi huo pia unapaswa kufafanua wazi namna utakavyochangia katika maendeleo na ustawi wa jamii.

### 4.2 Mgawanyo wa gharama na faida miongoni mwa wadau katika biashara ya kaboni

Mifumo ya mgawanyo wa gharama na faida katika biashara ya kaboni itazingatia mtaji uliowekezwa, majukumu na wajibu wa wadau wa mradi. Aidha, ulipaji wa mgawanyo wa faida utazingatia mifumo ya serikali ya malipo iliyopo, mfano matumizi ya namba ya uthibiti (*control number)*.

#### 4.2.1 Mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida Tanzania Bara

Mgawanyo wa gharama na faida katika ya miradi ya biashara ya kaboni miongoni mwa wadau umeainishwa kwenye kanuni.

##### 4.2.1.1 Miradi inayohusisha matumizi ya ardhi

Kwa miradi inayohusisha matumizi ya ardhi:

a) Mmiliki atapata asilimia sitini na moja ya mapato ghafi yatokanayo na mauzo ya Viwango vya Kaboni vilivyothibitishwa.
b) Iwapo Mmiliki atakuwa chini ya halmashauri, asilimia kumi kati ya asilimia sitini na moja itapewa halmashauri kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ikijumuisha biashara ya kaboni;
c) Asilimia hamsini na moja inayobaki itatumiwa na serikali ya kijiji au mtaa kwa shughuli za maendeleo ya jamii na shughuli za uhifadhi katika ngazi ya kijiji au mtaa;
d) Iwapo Mmiliki hayupo chini ya mamlaka ya halmashari asilimia kumi kati ya asilimi sitini na moja itatumiwa kwa shughuli za jamii katika ngazi ya kijiji au mtaa. Ambapo asilimia sita itapelekwa kwa vijiji vya jirani au mtaa na asilimia nne itapelekwa kwa halmashauri kwa shughuli za uhifadhi na asilimia hamsini na moja iliyobaki atapewa Mmiliki;
e) Mpendekezaji atalipa asilimia tisa kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa kati ya asilimia thelathini na tisa iliyobaki kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili; na
f) Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa atalipa asilimia mbili kati ya asilimia tisa kwenye mfuko wa mazingira, asilimia moja kati ya asilimia Saba zilizobaki atalipa kwa wakala anayesimamia nishati kwa ajili ya kulipia sehemu ya gharama za nishati ya kupikia. Asilimia sita zilizobaki zitatumiwa na Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa katika shughuli za usimamizi, udhibiti na uendelezaji wa biashara ya kaboni nchini.

##### 4.2.1.2 Miradi ya aina nyingine

Kuhusiana na miradi ya aina nyingine kama vile inayohusu udhibiti wa taka, matumizi ya nishati na uzalishaji viwandani ambapo gharama za uwekezaji ni za juu, mgawanyo wa gharama na faida utategemea makubaliano kati ya Mmiliki na Mpendekezaji wa mradi.

#### 4.2.2 Mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida Zanzibar

Endapo mradi wa biashara ya kaboni utatekelezwa Zanzibar, mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida utaamuliwa kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa na Mamlaka ya Usimamizi.

## SURA YA TANO

## 5.0 MFUMO WA KITAASISI

Utekelezaji wa miradi ya Biashara ya Kaboni unahusisha ushiriki na ushirikiano wa wadau mbalimbali katika ngazi za jamii, kitaifa na kimataifa, kuanzia serikali, sekta binafsi na asasi zisizo za serikali.

Katika ngazi ya kimataifa, Mkutano wa Nchi Wanachama ni chombo cha juu cha uamuzi katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Itifaki ya Kyoto ilianzisha mfumo wa Miradi ya Maendeleo ya kupunguza gesijoto chini ya usimamizi wa Mkutano wa Nchi Wanachama ambao ulianzisha Bodi ya Miradi ya Maendeleo ya kupunguza gesijoto ili kutoa mwongozo kwa miradi ya kaboni.

Aidha, Makubaliano ya Paris yalianzisha mfumo wa hiari wa upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto na kuchochea maendeleo endelevu chini ya usimamizi wa Mkutano wa nchi wanachama.Vilevile, Mkutano wa nchi wanachama ulianzisha chombo cha usimamizi ili kusimamia utekelezaji wa mfumo huo ambao utaongozwa na kanuni na taratibu zilizoandaliwa.

Katika ngazi ya kitaifa, usimamizi wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi upo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar.

Kuhusiana na miradi ya biashara ya kaboni katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, majukumu ya wadau muhimu yamebainishwa katika Kiambatisho 1.

## VIAMBATISHO

***Kiambatisho Na 1: Majukumu ya wadau muhimu kwenye biashara ya kaboni nchini***

1. **Majukumu ya Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa yatajumuisha-**
    a. kuunganisha nchi na michakato ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi;
    b. kuratibu masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi nchini;
    c. kutoa miongozo ya kisera kuhusu biashara ya Kaboni na kuweka mifumo mingine ambayo inakuza haki ya uwekezaji, jamii, utamaduni, uchumi na mazingira;
    d. kutoa barua ya kukubali usajili wa mradi wenye sifa;
    e. kusajili miradi ya biashara ya kaboni chini ya mfumo wa soko la kimtaifa na soko huria;
    f. kuunda Kamati ya Wataalam ya Kitaifa ya Tathimini kwa ajili ya kuhakiki na kuchambua wazo la mradi;
    g. kuidhinisha andiko la mradi;
    h. kumshauri mpendekezaji wa mradi kuzingatia sera za bima kwenye miradi ya kaboni;
    i. kutoa taarifa muhimu kwa mpendekezaji wa mradi wa biashara ya Kaboni;
    j. kupima, Kutoa taarifa na kuhakiki gesijoto;
    k. kuratibu na kufanya ufuatiliaji na tathimini ya miradi iliyosajiliwa ya biashara ya Kaboni;
    l. kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya mazingira katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa masuala yanayohusu biashara ya kaboni;
    m. kutunza rejesta ya miradi yote ya biashara ya Kaboni nchini; na
    n. kutekeleza mambo yote muhimu kwa mujibu wa Kanuni na mikataba ya kimataifa.

2. **Kuhusiana na miradi ya biashara ya kaboni Zanzibar, Mamlaka ya Usimamizi itakuwa na majukumu yafuatayo**:
    a. kuratibu usimamizi wa mazingira na shughuli zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi Zanzibar;
    b. kushirikiana na Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa kwenye masuala ya biashara ya kaboni;
    c. kutoa miongozo ya kisera kuhusu biashara ya Kaboni na kuweka mifumo mingine ambayo inakuza haki ya uwekezaji, jamii, utamaduni, uchumi na mazingira;
    d. kutoa barua ya kukubali usajili wa mradi wenye sifa kwa miradi itakayotekelezwa Zanzibar;
    e. kuweka rejista ya miradi yote ya biashara ya kaboni Zanzibar;
    f. kutoa Barua ya kuidhinishwa kwa Andiko la Mradi wenye sifa;
    g. kuratibu na kufanya ufuatiliaji na tathimini ya miradi iliyosajiliwa ya biashara ya Kaboni;
    h. kusimamia miradi/programu zilizosajiliwa kwa ajili ya biashara ya kaboni;

i. kujenga uwezo na uhamasishaji juu ya biashara ya kaboni;
j. Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kugawana gharama na faida;
k. kuunda Kamati ya Wataalam ya Kitaifa ya Tathimini kwa ajili ya kuhakiki na kuchambua wazo la mradi Zanzibar;
l. Kutoa taarifa muhimu kwa Mpendekezaji anayetaka kufanya biashara ya kaboni Zanzibar; na
m. kutekeleza mambo yote muhimu kwa mujibu wa Kanuni na mikataba ya kimataifa

3. **Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itakuwa na majukumu yafuatayo:**
   a. kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera na miongozo kuhusu miradi ya biashara ya kaboni;
   b. kutoa maelekezo kuhusu mapato na matumizi yanayohusiana miradi ya biashara ya kaboni;
   c. kuwezesha kujenga uwezo katika biashara ya kaboni;
   d. kupitia mikataba na hati za makubaliano zinazohusu biashara ya kaboni; na
   e. kuhakikisha kuwa shughuli za uhifadhi wa mazingira zinapewa kipaumbele kwenye matumizi ya mapato yanayotokana na miradi ya kaboni.

4. **Wizara za kisekta (Tanzania Bara na Zanzibar) zitakuwa na majukumu yafuatayo:**
   a. kutoa ushauri wa kitaalamu, usimamizi na kisheria kwenye biashara ya kaboni;
   b. kutoa barua ya ridhaa kwa mradi wa biashara ya kaboni uliopendekezwa katika sekta husika; na
   c. kutambua Kiwango cha Kaboni kilichoidhinishwa kutoka katika miradi ya biashara ya kaboni inayotekelezwa katika sekta husika kwenye tathmini ya taifa ya gesijoto.

5. **Mmiliki atakuwa na majukumu yafuatayo:**
   a. kuandaa na kutekeleza mradi kama Mpendekezaji au mbia wa Mpendekezaji
   b. kutoa ushahidi wa umiliki wa mali inayohusika katika mradi wa biashara ya kaboni;
   c. kuandaa, kusaini na kutekeleza mikataba inayohusiana na miradi ya biashara ya kaboni; na
   d. kutoa barua ya ridhaa kupitia mamlaka ya serikali inayohusika kuthibitisha ushiriki katika mradi wa biashara ya kaboni

6. **Mpendekezaji atakuwa na majukumu yafuatayo:**

   a. kusajili mradi wa biashara ya kaboni kwa Msajili;
   b. kuandaa na kutekeleza mradi wa biashara ya kaboni;
   c. kushauriana na Mmiliki husika na wadau wengine wowote katika kuandaa na kutekeleza mradi wa kaboni;
   d. kuandaa na kuingia mikataba na wadau katika utekelezaji wa miradi ya biashara ya kaboni;
   e. kuuza Viwango vya Kaboni vilivyozalishwa na mradi wa kaboni;

f. kugawa mapato yanayotokana na mauzo ya Viwango vya Kaboni kwa wadau kwa kuzingatia mfumo wa mgawanyo wa gharama na faida kwa mujibu wa kanuni ya 33;
g. (g) kuandaa na kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa biashara ya kaboni kwa mujibu wa kanuni ya 41 kwa kushirikiana na mamlaka ya serikali husika, Mmiliki au mbia; na
h. (h) kujenga uwezo wa wadau katika biashara ya kaboni.

**7. Sekretarieti ya mkoa itakuwa na majukumu yafuatayo:**

a. kusimamia na kuratibu miradi ya biashara ya kaboni katika eneo lake la kiutawala;
b. kuwezesha kujenga uwezo kuhusu biashara ya kaboni katika ngazi ya mkoa, mamlaka za serikali za mitaa na jamii; na
c. kutoa ushauri wa kitaalamu, usimamizi na kisheria kwenye biashara ya kaboni

**8. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakuwa na majukumu yafuatayo:**

a. kusimamia miradi ya biashara ya kaboni katika maeneo yao ya kiutawala, kwa kushauriana na sekretarieti ya mkoa;
b. kupitia na kuchambua miradi ya biashara ya kaboni katika ngazi ya halmashauri;
c. kuhakikisha maslahi ya jamii inayozunguka mradi yanalindwa katika miradi au programu za biashara ya kaboni;
d. kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya biashara ya kaboni katika maeneo yao ya kiutawala;
e. kuandaa na kutekeleza miradi au programu kama Mpendekezaji mtarajiwa katika maeneo yao ya kiutawala;
f. kukusanya mirabaha ya kisheria iliyopatikana kutoka kwenye miradi au programu za biashara ya kaboni katika maeneo yao ya kiutawala;
g. kuwezesha kujenga uwezo wa jamii inayozunguka mradi wa biashara ya kaboni na viongozi wa vijiji;
h. kutoa miongozo inayofaa kuhusu uandaaji wa mipango, bajeti na matumizi ya fedha za miradi ya biashara ya kaboni; na
i. kutoa ushauri wa kitaalamu, usimamizi na kisheria kwenye biashara ya kaboni katika maeneo yao ya kiutawala.

**9. Serikali ya kijiji au mtaa itakuwa na majukumu yafuatayo:**

a. kuandaa, kusaini na kusimamia utekelezaji wa mikataba inayohusiana na miradi ya biashara ya kaboni kwa kushauriana na halmashauri husika;
b. kulinda maslahi ya jamii inayozunguka miradi ya biashara ya kaboni;
c. kuhakikisha ushiriki wa jamii inayozunguka mradi wa biashara ya kaboni;
d. kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa biashara ya kaboni katika kijiji au mtaa;
e. kuandaa na kutekeleza mradi wa biashara ya kaboni kana Mpendekezaji mtarajiwa;
f. kuhakukisha ushiriki wa umma katika kujenga uwezo kuhusu biashara ya kaboni; na

g. kuandaa mipango, bajeti, matumizi na kutoa taarifa za fedha katika miradi ya biashara ya kaboni katika kijiji au Mtaa.

**10. Ssekta binafsi, washirika wa maendeleo na asasi za kiraia, zitakuwa na majukumu yafuatayo:**

a. kupanga, kuandaa na kutekeleza miradi au programu za kaboni;
b. kufanya tafiti katika biashara ya kaboni;
c. kuwezesha kujenga uwezo katika biashara ya kaboni; na
d. kuhamasisha upatikanaji wa fedha za kaboni.

**11. Majukumu ya Baraza kuhusiana na miradi ya biashara ya kaboni yatakuwa kama ifuatavyo: -**

a. kuhakikisha uzingatiaji na utekelezaji wa sheria katika miradi ya biashara ya kaboni; na
b. kutoa elimu kuhusu biashara ya kaboni.

**12. Majukumu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) ni pamoja na-**

a. kuhakikisha uzingatiaji na utekelezaji wa sheria katika miradi ya biashara ya kaboni; na
b. kutoa elimu kuhusu biashara ya kaboni.

**13. Kamati ya Wataalamu ya Kitaifa/Zanzibar ya Kutathmini Miradi ya Kaboni itakuwa na majukumu yafuatayo:**

a. Kufanya uchambuzi wa Andiko la Awali la Mradi kama litakavyowasilishwa kwake na kutoa mapendekezo kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa;
b. kufanya uchambuzi wa Andiko la Mradi kama litakavyowasilishwa kwake na kutoa mapendekezo kwa Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa; na
c. kutekeleza majukumu mengine yoyote yanayoweza kuwasilishwa kwake na Mamlaka ya Taifa ya Uratibu au Mratibu wa Kitaifa chini ya Kanuni hizi.